

JINA: NAMBARI:

SHULE: TAREHE:

SAHIHI:.....

102/2

KISWAHILI

LUGHA

KARATASI YA PILI

JULAI / AGOSTI 2014

MUDA: SAA 2½

MTIHANI WA MWIGO WA WILAYA YA NANDI KASKAZINI 2014

Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari

KISWAHILI

LUGHA

KARATASI YA PILI

MUDA: 2½

MAAGIZO

1. Andika **jina lako** na **nambari yako** ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
2. Tia **sahihi** yako kisha **uandike tarehe** ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
3. Jibu maswali **yote**.
4. Majibu **yote** yaandikwe katika nafasi zilizoachwa katika kijitabu hiki cha maswali.
5. *Usitoe* ukurasa wowote kutoka kwenye kijitabu hiki.
6. Watahaniwa ni lazima wahakikishe kwamba kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.

Kwa matumizi ya mtahini pekee.

Swali	Upeo	Alama
1	15	
2	15	
3	40	
4	10	
JUMLA	80	

1. **UFAHAMU (ALAMA 15)**

Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali.

Kweli, taarifa zimeonekana katika vyombo vya habari kuwa vijana wetu wanajua mengi kutushinda. Wengi wameshiriki ngono ilhali tukiwa nyumbani sisi wazazi tunawaona kuwa malaika.

Kwa kweli taarifa hizo ni sawa na mbiu ya mgambo kuwa tuzungumze na watoto wetu kuhusu suala hili. Ni vyema wajue kutoka kwetu kuliko kufahamu kutoka kwa wengine ambao badala ya kuwaelekeza wanawapotosha. Mara nyingi wakiwa katikati ya marika, wao hushinikizana kujaribu na wengi wanaamini kuwa kufanya mara moja si tatizo. Lakini kile ambacho hawaelewi ni kuwa hiyo mara moja inaweza kuwabelesha mimba ama kuwaambukiza ukimwi na maradhi ya zinaa. Aidha, utu huumbuliwa na hivyo kupotoka kimaadili. Hayo ni masuala ambayo wazazi hawafai kuyaonea haya tena kwa sababu watoto wetu wanayafahamu lakini cha msingi ni kujua ukweli na hatari zilizopo.

Wazazi wengi wamewatelekeza watoto wao. Wengi husema kuwa wanawatimizia kila hitaji. Hii inamaanisha kuwa unalipa karo kwa wakati unaofaa, kuna chakula cha kutosha nyumbani, mavazi wako nayo na pia pesa za mfukoni wanazo. Lakini kile ambacho hawana ni muda wa kuwa na watoto wao. Baadhi ya matatizo tunayokumbana nayo yanaweza kutatuliwa ikiwa wazazi watatenga muda wa kuzungumza ana kwa ana na watoto wao.

Ni kweli wengi wamesingizia kazi zao kwa sababu wanaamka mapema na kurudi usiku. Lakini hiyo kazi ina maana gani ikiwa kesho utajipata na mjukuu wa kulea bila kutarajia? Kwa hivyo, wazazi lazima waache kuwaachia wafanyakazi wa nyumbani jukumu lao ama kuwapeleka katika shule za bweni mapema kwa sababu wanawaona kuwa mzigo. Pia kuna wale ambao huwachwa hata vilabuni kwa madai kuwa wanakutana tu na marafiki zao.

Baadhi ya mavazi, ingawaje huwafanya watoto wao kuonekana kama wanaoenda na wakati ama ya kisasa, huwa hayafai. Lazima wafunzwe tangu wakiwa wachanga kuhusu suala la kujiheshimu. Haifai kufikiria kwamba kwa sababu ni mtoto anaweza kuvaa chochote kile. Mtoto anafaa kuvishwa mavazi ya heshima. Pia, wazazi wachunguze mavazi yao wenyewe.

Maswali

- (a) Eleza dhamira ya mwandishi wa makala haya. (alama 2)

.....
.....

- (b) Kushiriki ngono mapema kwa vijana kuna athari gani kilingana na makala haya?

(alama 4)

.....
.....
.....
.....

(c) Wazazi wamechangia vipi shida zinazokumba vijana chipukizi? (alama 4)

.....
.....
.....
.....

(d) Taja majukumu manne makuu ya mzazi kulingana na makala haya. (alama 4)

.....
.....
.....

(e) Eleza maana ya maneno haya kimuktadha.

(i) Madai (alama1)

.....
.....

(ii) Mbui ya mgambo (alama1)

.....
.....

2. UFUPISHO: (ALAMA 15)

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.

Sekta za umma humu nchini hazina kifani katika uzembe. Unapohitaji huduma za posta, umeme, maji, mawasiliano, utayarishaji wa mishahara na malipo mengine, utalazimika kusubiri kwa siku, miezi na hata miaka ili upate haki yako, hata wakati mwingine ukakosa!

Wafanyakazi wa sekta hii hukosa kutimiza majukumu yao ipasavyo kutokana na ukosefu wa motisha yaani mishahara duni, uhaba wa nyenzo za kutekeleza majukumu yao na kutozingatia kazi kwa wakaguzi na viongozi wa wafanyikazi.

Minghairi ya hali hii, visa vya ufiadini ndiyo sifa inayopambanua huduma za umma. Baadhi ya wafanyakazi hupatikana maofisini na katika maeneo yao ya kikazi kwa nadra sana kwa sababu hukimbilia kwingineko kutafuta malipo ya kujazia mishahara yao duni kujikimu kimaisha. Athari za matendo haya zimekuwa kukokota kukua kwa uchumi, ukosefu wa imani kwa huduma za umma na utoaji wa huduma hafifu.

Kufuatia udhaifu huu, katika siku za majuzi, sekta za kibinafsi zimetambulika kuwa muhimu sana katika utoaji huduma kwa wananchi. Uchumi wa mataifa yanayopendelea sekta za kibinafsi yametambuliwa kukua kwa kasi kuliko yale yanayoandama mfumo kongwe wa serikali kutawala shughuli za uzalishaji mali.

Lakini kwa kuwa mashirika ya kibinafsi, aidha, yamebainika kuwa na udhaifu wa aina yake, serikali inaposhirikiana kindakindaki na sekta hii, uwastanishaji wa hali za kazi utajiri. Kwa kuwa dhamira kuu ya mashirika ya kibinafsi huwa kujizolea faida kemkem, yamekuwa yakifanyisha wafanyikazi wao kazi nyingi kupita kiasi ambayo mara nyingine huwadhuru kiyafya. Japo mishahara wao ni afadhali kuliko wa sekta ya umma, baadhi ya sera huwa kandamizi na hutinga fursa za wafanyikazi kukuza

majukumu yao binafsi, mengi yakiwa muhimu kwa jamii jumla.

Ushirikiano wa serikali na mashirika ya kibinafsi, kwa hivyo, una uwezo mkubwa wa kustawisha na kupanua mawanda ya uchumi. Utakuwa dawa mujarabu kwa udhaifu wa pande zote. Sekta za kibinafsi zinazolenga kujipatia faida nyingi, kwa upande mmoja, zitasaidia katika kuondoa uzembe, utepetevu na mapuuza yanayotamalaki huduma za serikali kwani yatalenga uzalishaji mwingi ili kutimiza malengo yao.

Maswali

(a) Eleza mawazo muhimu ya aya tatu za kwanza kwa maneno 50-55.

(alama 6, 1 utiririko)

Matayarisho

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

Nakala safi

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....
Fupisha aya tatu za mwisho bila kubadilisha maana iliyokusudiwa kwa maneno
75 – 80. (alama 8, 1 utiririko)

Matayarisho

.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....

Nakala safi

.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....

.....
3. **MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)**

(a) Ainisha sentensi ifuatayo (alama 3)

Aliyempenda

.....
.....
.....

(b) Eleza matumizi ya viambishi 'ki' na 'na' katika sentensi hizi (alama 2)

(i) Uji bila sukari haunyweki.

.....

(ii) Wizi ule uliongozwa na Wanugu.

.....

(c) Eleza maana **mbili** za sentensi hii; wizi wa silaha umeongezeka. (alama 2)

.....
.....
.....

(d) Nyambua vitenzi vifuatavyo katika hali zilizo kwenye mabano. (alama 2)

(i) Tua (Tendama)

.....

(ii) Fumba (Tendata)

.....

(e) Bainisha vielezi na ueleze ni vya aina gani. (alama 2)

(i) Ngozi imenyooka twaa:.....

.....

(ii) Arusi iliahirishwa hadi baadaye:.....

.....

(f) Changanua hii sentensi kutumia jedwali. (alama 4)

Rehema ambaye huimba taarab ni mwanamke mpole.

- (g) Tunga sentensi mbili kutofautisha vitate hivi kimaana. (alama 2)
 (i) Hawara:.....

 (ii) Hawala:.....

- (h) Andika kwa wingi (alama 2)
 Zigo lile la kuliwa halilemei

- (i) Geuza kwa ukubwa (alama 2)
 Msichana mweusi anasoma kitabu.

- (j) Tumia viashiria vya kuthibitisha kujaliza pengo (alama 2)
 (i) Tingatingahuegeshwa hapa kila siku
 (ii) Maarifa.....ndiyo yaliyomfanikisha
- (k) Kanusha bila kutumia 'amba' (alama 2)
 Nitavaa nguo ambayo ni safi

- (l) Andika nomino moja moja yenye sauti zifuatazo. (alama 2)
 (i) Kizuio – kwamizo

 (ii) Kimadende

- (m) Bainisha aina za yambwa na chagizo (alama 3)
 Mkulima alivuniwaa mahindi mwezi uliopita.

- (n) Geuza sentensi iwe katika wakati uliopita, hali timilifu (alama 1)
 Aliomba msamaha kwa kuchelewa.

- (o) Andika sentensi hii katika usemi halisi (alama 2)
 Amina alishangaa na kutaka kujua ni nani aliyekuwa amekila chakula chake.

.....
.....
(p) Taja aina za mofimu na kuzitolea mifano (alama 2)

.....
.....
(q) Eleza matumizi **mawili** ya alama ya ritifaa. (alama 2)

4. **ISIMU JAMII (ALAMA 10)**

Lugha ya magazeti ina upekee wake. Fafanua sifa **tano** kisha ueleze upekee huu hukusudia nini. (alama 10)

.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....